

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)



## MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 07 mwezi 02 2022

### KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA DSM, S.L.P. 40274,  
DAR-ES-SALAAM ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya  
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana  
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

RASHID WAZIRI GHAFUZ S.L.P. \_\_\_\_\_, MOMBO KOROGWE  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya  
PANGANI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za  
njie kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya PANGANI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya  
KUSIKI NA KUPAKA RANGI JENGO LA MADARASA  
(GENERAL CLASS ROOM)

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo  
wa vifaa vya Ujenzi (Schedule of materials) vinavyoonyesha namna kazi  
itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

## **1. GHARAMA YA UFUNDI**

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 2,300,000, Fundi atafanya kazi ya KUSUMA NA KUWA LA kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu. Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

## **2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)**

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

## **3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundi.

## **4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

(a) Fundi atakabidhiwa eneo la kazi tarehe 21 mwezi 02 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

(b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

(c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

## **5. WAJIBU WA FUNDI**

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi (arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA

Jina:

Uathim Juma

Saini:

T :

Wadhifa:

Atew'

Tarehe:

07/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina:

Fanda R. Allute

Saini:

R. Allute

Wadhifa:

Mhandisi wa Mudi

Tarehe:

07/02/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina:

RASHID GHAFUR

Mbele ya

Wadhifa:

FUNDI

Saini:

Rashid

Tarehe:

07/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina:

SAID NAREJA

Saini:

S. Nareja

Wadhifa:

Dundi

Tarehe:

7.2.2022